



TAARIFA KWA UMMA

ZOEZI LA USAJILI WATUMIAJI HUDUMA YA MAJI BILA KIBALI

Shirika la MajiSafi na Majitaka Dar-es-salaam (**DAWASCO**), inawatangazia wakazi wote wa jiji la **Dar es salaam** na Miji ya **Bagamoyo** na **Kibaha** Mkoani **Pwani** kuwa zoezi la usajili kwa waliojiunganishia huduma ya Maji bila kibali cha shirika limeanza rasmi kwa kipindi cha miezi miwili kuanzia **Agosti** mpaka **Septemba, 2018**.

Hivyo wananchi ambao wamejiunganishia huduma ya Maji bila kibali, shirika linawataka kufika katika Ofisi yoyote ya Dawasco iliyo karibu kwa ajili ya kusajiliwa na **usajili** utafanyika **bure** bila faini yoyote kwa kipindi hichi.

Aidha baada ya zoezi la usajili kukamilika kutakuwa na msako mkali wa nyumba kwa nyumba na wananchi watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwemo kufikishwa mahakamani kwa kosa la kuhujumu uchumi.

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja **0800110064** (**BURE**).

IMETOLEWA NA:

OFISI YA UHUSIANO

DAWASCO-MAKAO MAKUU